

Toleo la Habari

Elimu na Makuzi ya Awali ya Watoto

Wanafunzi wa sekondari ngazi ya juu kutumia vifaa vyao binafsi vya kielektroniki; programu ya kusaidia familia za kipato cha chini na kati

Julai 22, 2020

FREDERICTON (GNB) – Wanafunzi wa shule za sekondari ngazi ya juu sasa watahitajika kuja na vifaa binafsi vya kielektroniki kwa ajili ya ujifunzaji kuanzia mwezi Septemba kama sehemu ya kuhamia kwenye muundo wa ujifunzaji ambao ni binafsi, shirikishi, na unaotumia zaidi teknolojia.

“Mazingira ya ujifunzaji yatakuwa tofauti katika kipindi cha mwaka wa shule wa 2020-21 na kadri tunavyoendelea kuishi katika kipindi cha gonjwa-tandavu la COVID-19,” alisema Dominic Cardy, Waziri wa Elimu na Makuzi ya Awali ya Watoto. “Muundo huu utasaidia kuunga mkono ujifunzaji changamano na mwendelezo wa ujifunzaji wa wanafunzi wa sekondari ngazi ya juu katika siku za usoni, huku pia ukishughulikia masuala yaliyokuwepo kwa muda mrefu.”

Idara hii inawekeza dola milioni 7 ili kuboresha ufikio wa teknolojia unaozingatia usawa na dola milioni 5 kwenye miundombinu ili kutegemeza muundo huu mpya wa ujifunzaji. Uwekezaji wa miundombinu utaunga mkono hitaji la ongezeko la muunganisho na ushirikiano wa kidijitali. Hii inajumuisha ongezeko la maeneo ya ufikio shuleni na maboresho ya ngome (firewall) na kipimo-data (bandwidth) shuleni. Uwekezaji huu utaunga mkono [Mpango wa Rudi Shuleni](#).

Muundo huu unawezesha wanafunzi kutumia vifaa wanavyovimiliki huku njia wanaztumia kujifunza na kuingiliana zikifanywa za kisasa. Unawapa pia walimu uhuru wa kutumia teknolojia ili kuvumbua na kuboresha ujifunzaji wa wanafunzi.

Programu ya kutoa ruzuku itapatikana kwa wanafunzi kutoka kwenye familia za kipato cha chini na cha kati ambao kwa sasa hawamiliki kifaa chochote. Familia zitapewa mpaka dola 600 kwa kila mwanafunzi wa sekondari ngazi ya juu ili kununua kompyuta mpakato kupitia programu hii, kulingana na sifa zao.

Sifa:

- Kaya zenye kipato cha mwaka cha hadi dola 40,000 zitapokea vocha ya dola 600 kwa kila mwanafunzi.
- Kaya zenye kipato cha mwaka cha kati ya dola 40,000 na dola 55,000 zitapokea kiasi kisichozidi vocha ya dola 400 kwa mwanafunzi wao wa kwanza na dola 600 kwa kila mwanafunzi wa ziada.
- Kaya zenye kipato cha mwaka cha kati ya dola \$55,000 na dola \$70,000 zitapokea kiasi kisichozidi vocha ya dola \$200 kwa mwanafunzi wao wa kwanza na dola \$400 kwa mwanafunzi wa pili na dola \$600 kwa kila mwanafunzi wa ziada.
- Kaya zenye kipato cha mwaka cha kati ya dola \$70,000 na dola \$85,000 zitapokea kiasi kisichozidi vocha ya dola \$200 kwa mwanafunzi wao wa pili, dola \$400 kwa mwanafunzi wa tatu na dola \$600 kwa kila mwanafunzi wa ziada.

Familia zenye sifa zitaweza kutuma maombi kupitia [Portal ya Wazazi mtandaoni](#) ifikapo Julai 31. Maelezo zaidi kuhusu programu hii yatatolewa moja kwa moja kwa familia. Maulizo yanaweza kufanywa kwa kupiga nambari 1-833-901-1963.

“Lengo letu ni kumweka kila mwanafunzi katika nafasi ya mafanikio kwa kuwaandaa kwa mafaniko ya muda mrefu katika elimu yao na mahala pa kazi pia kuhakikisha ufikio wa teknolojia unaozingatia usawa na udumifu,” alisema Cardy.

Majukwaa ya ufundishaji mtandaoni yamebainishwa ili kuunga mkono ujifunzaji kwa wanafunzi wa sekondari ngazi ya juu na yatatumika kwa ajili ya mafundisho ya kila siku. Microsoft Teams itakuwa jukwaa kuu litakalotumika darasani, ambalo wanafunzi na walimu wanaweza kulifikia kupitia akaunti zao za Office 365.

Baadhi ya walimu wanaweza pia kuchagua kutumia Desire 2 Learn, inajulikana pia kama Brightspace, katika sekta ya Kiingereza au Clic katika sekta ya Kifaransa. Masharti ya mifumo ya majukwaa haya [yanapatikana mtandaoni](#) na familia zinahimizwa kuzipitia nyaraka hizi ili kuthibitisha utangamanifu (compatibility) wa vifaa vya wanafunzi wao.

“Kuwapa wanaunzi chaguzi za uzoefu wa ujifunzaji ambao ni binafsi zaidi na ambao unakidhi mahitaji na uwezo wao ni kipengele muhimu cha kuunda mfumo wa elimu wenye hadhi ya kimataifa,” alisema Cardy.

Kutoa ufikio wa teknolojia ya habari na mawasiliano unaozingatia usawa ni jamo lililopo kwenye [Mpango wa Elimu wa Miaka 10: Kila mtu katika ubora wake](#). Kuunga mkono sera za “njoo na kifaa chako”, kuweka sheria za jimbo kwa ajili ya upatikanaji na utumiaji wa teknolojia na kushughulikia suala la ukosefu wa usawa wa teknolojia ni mambo ya kuchukuliwa hatua yaliyoainishwa katika [Kufanikiwa Nyumbani: Waraka wa majadiliano kuhusu Elimu katika New Brunswick](#), ambao unaunga mkono mipango ya elimu ya miaka 10.

Mawasiliano ya Habari

Danielle Elliott, mawasiliano, Idara ya Elimu na Makuzi ya Awali ya Watoto, danielle.elliott@gnb.ca.